# THE EMBASSY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**Telephone: +(257) 22 248636**
**Fax : +(257) 22 248637**
**E-mail : tanzanrep@usan-bu.net**

**Kinindo**
**Avenue Du Large,**
**House No. 51,**
**B.P 855,**
**BUJUMBURA,**
**BURUNDI.**

**Kumb.Na. CHAB 357/448/01/9** **09 Machi, 2020**

**Watanzania wote waishio Burundi**

**YAH: TAHADHARI DHIDI YA VIRUSI VYA CORONA**

Ndugu Watanzania wote mliopo nchini Burundi, kama mnavyofahamu, virusi vya Corona vinavyosababisha ugonjwa uitwao Covid19 unaendelea kusambaa katika nchi mbali mbali duniani zikiwemo Korea Kusini, Italia na Iran. Kwa bara la Afrika, tayari ugonjwa huo upo katika nchi za Misri na Senegal. Ugonjwa huo ambao ulianzia nchini China katika jimbo la Wuhan, hauna tiba maalumu.

Tarehe 18 Februari, 2020 Serikali ya Burundi, kupitia kitengo chake cha kupambana na magonjwa ya maambukizi au magonjwa ya mlipuko kilichopo chini ya Wizara ya Afya, kilitoa tamko rasmi kuhusiana na virusi vya Corona ambapo imesema hadi sasa hakuna mtu yeyote aliyeambukizwa virusi vya Corona nchini Burundi. Hata hivyo, ni vyema na sisi wenyewe tuendelee kuchukua tahadhari kwa kadri inavyowezekana. Aidha, Ubalozi unashauri tuendelee kuchukua tahadhari zifuatazo:-

i. Licha ya ugonjwa huo kuwa hatari, hakuna haja ya kuwa na hofu ya kupita kiasi na badala yake ni vema tuendelee kuwa katika hali ya utulivu.
ii. Itakapobidi zichukuliwe tahadhari za kunawa mikono kwa sabuni na kuepuka kukaribiana sana na kusalimia kwa kushikana mikono.
iii. Tuepuke kwenda maeneo yenye misongamano mikubwa ya watu.
iv. Tufuatilie na kutekeleza tahadhari zote zitakazokuwa zinatolewa na serikali ya Burundi na kwenye mitandao, magazeti na televisheni.

Kama itatokea Mtanzania yoyote kukumbwa na ugonjwa huo, Ubalozi unaomba kujulishwa mapema.

**Ubalozi wa Tanzania, Bujumbura**
09 Machi, 2020